



WIKI YA ASASI ZA KIRAIA 2018

Tarehe: 22- 26 Oktoba 2018 | Mahali: Dodoma, Tanzania

BARUA YA MWALIKO

Taasisi ya Foundation for Civil Society (FCS) kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya Asasi za Kiraia nchini wameandaa Wiki ya Asasi itakayofanyika Dodoma kuanzia tarehe 22 hadi 26 Oktoba, 2018. Wiki hii linatarajiwa kuzileta pamoja asasi zaidi ya 300 kutoka Tanzania bara na visiwani, kwa lengo la kuzikutanisha na wadau wa maendeleo ikiwemo Wizara, Idara na wakala wa Serikali, Bunge, wahisani wa sekta binafsi n.k

Yafuatayo ni matukio muhimu katika Wiki ya Asasi za Kiraia 2018

□ Warsha na makongamano:

Mada mbalimbali zitawasilishwa ili kutoa fursa kwa washiriki, kujifunza na kubadilishana uzoefu na wadau wa maendeleo kutoka sekta mbalimbali. Aidha washiriki watapata fursa ya kuhudhuria warsha zenye mada kuu pamoja na warsha za mada mahususi kwa sekta mbalimbali. Lengo ikiwa ni kuhakikisha ushiriki maridhawa wa wadau wote

Washiriki wanahimizwa kuchagua mada zenye umuhimu na manufaa kwa Asasi zao ili kuhakikisha ushiriki wao katika wiki hii ya Asasi za Kiraia nchini unaleta manufaa kwa taasisi zao.

□ Maonesho:

Wiki ya Asasi za Kiraia inatoa fursa kwa Asasi za kiraia nchini pamoja na wadau wa maendeleo kuhabarisha umma wa watazania shughuli na huduma wanazotoa kupitia Maonesho. Maelezo ya jinsi ya kushiriki katika maonesho yameambatanishwa.

□ Matamasha na burudani:

Kila siku wakati wa jioni washiriki watapata fursa ya kukutana, kubadilishana mawazo na kujenga mahusiano. Burudani mbalimbali zimeandaliwa ikiwemo matamasha ya kitamaduni na ngoma za kiasili, matamasha ya michezo pamoja na chakula cha jioni katika sherehe za kufunga wiki.

Ukiwa kama mshiriki mtarajiwa wa wiki hii, tafadhali soma kwa makini maelezo katika vitini vilivyo ambatanishwa kwenye mwaliko huu. Ukiwa na nia ya kushiriki jaza fomu ya usajili na kuirejesha kama ilivyoainishwa hapo chini.

1. Muhtasari kuhusu Wiki ya Asasi za Kiraia 2018
2. Ratiba ya Wiki ya Asasi za Kiraia 2018
3. Fomu ya usajili kwa washiriki katika warsha mbalimbali
4. Mwongozo kwa washiriki wa maonesho

Tafadhali wasilisha Fomu ya usajili iliyokamili kabla ya Tarehe 05 Oktoba, 2018.

Kwa mawasiliano zaidi: Barua Pepe: csoweeek2018@thefoundation-tz.org / Tovuti: www.thefoundation.or.tz

Simu : +255 762 767 237

Francis Kivanga | Mkurugenzi Mtendaji

